بسم الله الرحمن الرحيم

26/Safar/1427H=26March/2006 AD.Madinatul Rasuul s.a.w.-Saudi Arabia.
Makala namba 5.

# HII NDIYO DAAWA YETU

## JUU YA UFAHAMU WA SALAF SWALIH

## UHARAMU KUYAJENGEA MAKABURI

Amesema Swahaba mtukufu Jabir bin Abdillahi r.a;
[Amekataza Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w
kulipaka chokaa kaburi,na kulikalia**,na kulijengea** ].
Tazama sahihi muslim juzuu 3ukurasa62.

MUANDISHI;

ABUL FADHLI QASSIM MAFUTA QASSIM.

بسم الله الرحمن الرحيم

Ewe mola wetu ni zako wewe sifa njema zote,na shukrani zote, ni zako wewe sifa njema vile zinavyo lingana na utukufu wako,na ukubwa wako,ni zako wewe sifa njema mpaka uridhike,na pale unaporidhika, na baada ya kuridhika.

Na sala na salamu zimfikie kipenzi chetu,Mtume wetu Muhammad, na jamaa zake,na maswahaba zake wote,na walioiandama njia yao kwa wema mpaka siku ya malipo.

Ndugu muislamu!
Katika sehemu hii ya pili ya mfululizo wa makala zetu UHARAMU WA KUYAJENGEA MAKABURI. Tutazijadili hoja na dalili zilizotumika katika kulitetea jambo hili la haramu .

Vijana hao wa Msikiti wa Buguruni kwa Mnyamani walifanya jaribio la kutaka kuzipindisha dalili za kisheria ili kutumukia mradi wao.
Na hizi zifuatazo ni hoja zao kwa ufupi na majibu yake ya kielimu pamoja na kubainisha makosa ya kielimu;

**MAKOSA YA KIELIMU YALIYOMO KWENYE MAKALA HIYO;**

-Ama katika sehemu hii -Inshaallah- tutayataja makosa machache ya kielimu kati ya mengi,makosa ambayo ndiyo sababu ya kupatikana fatawa hizo za kimakosa,kwa kauli isemayo;

kila kinachozalikana na najisi basi nacho huwa ni najisi.

Kwahiyo kila kilicho jengwa juu ya msingi wa kimakosa basi nacho huwa ni makosa.
hapa tutalitaja kila kosa na kulipigia mstari kisha tutafuatishia jawabu yake kwa ufupi;

**kosa lake la kwanza;**

Ni pale waliposema katika ukurasa wa kwanza wa makala hiyo;

[..kwanza tuchukue maneno haya mawili mushrifan na sawwaitahu,tamko la al mushrif lina maana kitu kuwa juu na chenye kunyanyuka ukitazama katika kamusi ya lugha ya kiarabu munjid utakuta pamesemwa hivi…].

**jawabu yetu;**

Kosa hapa ni kuitegemea kamusi ambayo si tegemezi katika ulimwengu wa wasomi wa kiislamu,nayo nihiyo kamusi ya al mun'jid iliyo andikwa na wagalatia wa kanisa la catholic kule Lebanon!

swali; kwani sheikh huna kamusi za maulamaa wa kiislamu? Au kuna kitu umekikimbia?

Na ama kusema kwamba tamko 'mush'rifan' lina maana ya kitu kuwa juu,hapa tunasema maana hiyo ni kweli,lakini swali linakuja hivi,je kaburi ukilijengea utakua umeliinua juu au umelisawazisha sawa na ar'dhi?

Na je kuyanjengea makaburi ni jambo lililo amrishwa au ni jambo lililo katazwa?

Na kama ni jambo lililo katazwa ni wazi kwamba jambo hilo ni haramu na ni munkari,sasa je munkari huo wa kuyajengea makaburi ukitaka kuuondoa utauondoa vipi?

Ni kwa kuyapaka rangi na kuyatia marumaru au ni kwa kuyavunjilia mbali?
Sasa mnalia nini ukiondoshwa munkari huu? Au mna yenu?

**kosa lake la pili;**

Ni pale aliposema katika ukurasa huo huo wa kwanza;

[..na kuna neno lingine 'At taswiyya' kilugha halikuja kwa maana ya kubomoa kama ingekuwa limekuja katika maana ya kubomoa basi pangesemwa 'wala qabran illa sawwaitahu bil ardhi'.

**jawabu yetu ni kama ifuatavyo;**

amesema Imamu An nawawy;

**ويؤيد الهدم قوله: ولا قبرا مشرفا الا سويته...**

[na linaitiliwa nguvu (suala la) kuvunja-makaburi- na kauli yake {s.a.w.} wala -usiliwache -kaburi lililo nyanyuka juu ila umelisawazisha..].

Imamu An nawawy anasema kwamba hadithi hii inayosema 'walaa qabran mush'rifan..' inaliunga mkono na kulitilia nguvu suala la kuyavunja makaburi.

Sheikh wa kwa mnyamani yeye anasema hapana,hadithi hii haina maana hiyo,kwanini?
Eti kwasababu amesoma kwenye kamusi ya wa catholic al mun'jid akaona kwamba sawwaitahu haina maana ya kubomoa!na haya ndiyo matatizo ya lugha za kwenye al mun'jid kamusi ya kigalatia.

**Kosa lake la tatu;**

Ni pale aliposema;

[Lakini hadithi haikuja hivyo kwahiyo Sayidna Ally Bin Abi Twalib alikusudia yasawazishwe makaburi yaliyoinuliwa nasio kubomolewa, maana hadith imesema 'wala qabran illa sawaitahu'wala hadithi haikusema 'walla binaa qubbatan illa sawaitahuma yaani wala jengo au quba ila ulibomoe…].

**jawabu yetu ni kama ifuatavyo;**

hapa Imamu Shawkany anatujibia kwa kusema;

[katika hadithi hii kuna ushahidi mkubwa wa kulisawazisha kila kaburi lililo inuka juu zaidi ya kiwango cha kisheria…na miongoni mwa sampuli za kuinuka kwa kaburi ni kuinuka kimo chake,na kuweka kuba juu yake au msikiti….kwasababu hiyo,Mtume{s.a.w.}alimtuma Ally KUYAVUNJA MAKABURI..]

Je sheikh wa kwa mnyamani unasemaje?
Je umeifahamu kazi aliyotumiwa Ally {r.a.t} na Mtume{s.a.w.}?
Au bado unataka kuing'ang'ania al munjid?

## Kosa lao la nne;

[hadithi haikusema;'walla binaa qubbatan illa sawitahuma….].

Nikweli hadithi haikusema hivyo na wala haitosema hivyo katu, kwasababu anayesema maneno hayo ni Bwana Mtume s.a.w. na yeye ni muarabu aliyefasaha, bali ni bingwa wa mafasaha wote s.a.w. kwahiyo hawezi kuzungumza kiarabu kibovu kama hicho, na kosa hili ni miongoni mwa makosa ambayo yanadhihirisha wazi kwamba muandishi wa makala hii si msomi wa dini,na bila shaka wasomi wamefahamu hapo kosa liko wapi.
Basi tafadhali ndugu yangu tafuta kazi ya kufanya acha kuingilia kazi usizo na ujuzi nazo.

**فدع عنك الكتابة لست منها * ولو سودت وجهك بالمداد**

## Kosa lake la tano;

Katika mstari wa mwisho kabisa ya ukurasa huo huo wa kwanza,amesema hivi;
[ndio maana Imamu muslim na wenzie hadithi hii wakaiweka katika mlango Babu amri bitaswiyatil...]!

**Jawabu ni kama ifuatavyo;**

Inaonekana sheikh huyu hamjui pia ni nani aliyeiwekea milango sahihi muslim,kwasababu ya kuwa mbali na dawawini za sunna,Imamu muslim{r.a.} hakuiweka hadithi hii katika mlango huo,
kwasababu yeye siye aliyeiweka milango ya kitabu chake.Kazi hiyo imefanyika baada ya kufa kwake kwa kar'ne nyingi,kazi hiyo imefanywa na Imamu An nawawy,na yeye ndiye aliyesema hivi;

[Suala la kuvunja makaburi linatiliwa nguvu na hadithi hii].

Basi tanabahi usiseme usilolojua,kaa chini kwanza usome Sunna za Mtume {s.a.w.} kisha ndiyo usimame kuusemea umma,kwani hujui kwamba elimu ni kabla ya kauli na amali?

**Kosa lake la sita;**

Nipale aliposema katika ukurasa wa pili kuanzia mstari wa 12 kutoka juu;

[kwahiyo kilichoamrishwa ni kusawazisha makaburi na sio kubomoa majengo hay tunayojenga ili kuweka kumbukumbu za mawalii na maulamaa wetu.].

**jawabu ni kama ifuatavyo;**

amesema swahaba Jarir {r.a.};

[Amekataza Mtume wa Mwenyezi Mungu {s.a.w.} kulipaka chokaa kaburi,na kulikalia,na KULIJENGEA.].

Amesema Imamu Ibinul Qayyim {r.a.};
[na halikadhalika makuba yaliyojengwa juu ya makaburi yanapaswa kuvunjwa yote…].
Na amesema Imamu Ibin Kathir As shaafy {r.a.};
[asili ya kuabudu masanamu ni kupituka mipaka katika (kuyaadhimisha) makaburi na watu wake].

Ama kuhusu suala la kubomoa makaburi hilo tumelithibitisha kwa hoja na dalili katika jawabu tano zilizo tangulia,ama kuhusu suala hili la kuweka kumbukumbu za mawilii na maulamaa kwanza tunalijibu kwa kuuliza maswali haya yafuatayo;

1-Je hamkuona kumbukumbu nyingine za kuwawekea hao mawalii na maulama wenu ila kwa jambo la kumuasi Bwana Mtume {s.a.w.} ? au hizi hadithi na fatawa za maulamaa tulizo zitaja hapo hamzijui?
2-Je inakuwaje kulisawazisha kaburi lililo jengewa kuba au kuta juu yake?
a)ni kwa kulipaka rangi?
b)kuliwekea marumaru?c,kulivunja ? je Amirul muuminina Ally {r.a.} alitumwa kwa kazi gani kati ya hizo?

**kosa lake la saba;**

ni pale aliposema hivi;

[ama kwa upande wa sanad ya hadith ile ya Abul hayaj tuliyoanza nayo wamo wapokezi ambao wanawachuoni wa hadithi wamewatia kasoro
Habib bin abi Thabit
Waki'l
Sufiyan bin Athaur…].

**Jawabu yetu ni kama ifuatavyo;**

Ndugu yangu muandishi wa makala hii sheikh wa msikiti wa kwa mnyamani Buguruni-Dar es salaam amejiingiza katika fani nzito asiyo na ujuzi nayo kabisa,ndiyo sababu ya kutuletea mambo ya vichekesho hapa,kama alivyosema mshairi;

**أمور يضحك السفهاء منها**

**ويبكي من عواقبها اللبيب**

Haya hebu tuvishuhudie hivyo vichekesho;

Kwanza kabisa kwa mujibu wa maelezo yake hayo tuliyo yataja hapo anataka kutuambia kwamba hadithi hii si sahihi bali ni dhaifu kwahiyo haifai kuitumia jambo ambalo si kweli na kama si hivyo kwanini ameitaja is'nadi ya hadithi nakuanza kuwatia kasoro wapokezi wake?

Bali hilo amelisema wazi katika ukurasa wa mwisho wa makala yake kama tutakavyo litaja hilo katika mahala pake.

Na kama hayo ndiyo makusudio yake-kuidhoofisha hadithi hii-basi sisi tunasema kwamba; hadithi hii ni sahihi na wala haina shaka yoyote kwasababu zifuatazo;

1-hadithi hii ameitaja Imamu muslim katika kitabu chake kiitwacho al jaamius-swahihi maarufu kwa jina la sahihi muslim,na yeye hakutaja humo ila hadithi sahihi tupu,isipokuwa hadithi kama saba hivi wanawachuoni wa hadithi wamezitia makosa na hii si katika hizo.

2-hadithi hii wameisahihisha kundi kubwa la maulamaa wa hadithi miongoni mwao ni maimamu hawa;
Muslim,Tir'midhy,na al muhaddithul as'ri Sheikh al Albany.

3-hakuna hata mwanawachuoni mmoja aliyeidhoofisha hadithi hiyo,na kama yupo basi na amtaje.

4-haya tujaalie kwamba hao wapokezi wana kasoro,je kuna ulazima wa kudhoofika is'nadi kudhoofika matini yake? hebu rejeeni katika vitabu vya elimu ya mustalahul hadithi halafu utupe jawabu ya kweli.

Kisha akasema Sufiyani bin Athaur,hakuna mwana wachuoni anaeitwa kwa jina hili,huyu anaitwa Sufiyan Athaury,hakuna bin katikati,lakini huwenda hili likawa ni kosa la kiufundi.

**Kosa lake la nane;**

Ni pale aliposema;

[ameandika Ibin Hajar akimnukuu **Abuu Haban** asema 'kwahakika huyu Habib alikuwa mdanganyifu].

**Jawabu yetu;**

Amekosea aliposema Abuu Haban,sawa sawa ni Ibin Hibban,na si Abuu Habban,huyu ni Imamu mashuhuri katika fani ya hadithi,ni ajabu kuwa hajulikani na muhadithi  huyu wa Buguruni!

Lakini hapa kosa kubwa zaidi ni hayo maneno alivyo yatafsiri kimakosa,amesema Ibin Hibban 'kaana mudallisan'.

Nawauliza wasomi je katika istilahi ya wanawachuoni wa hadithi wakisema mtu fulani ni 'mudallisi'je wanamaanisha  kwamba ni kadhaabu (muongo)?

**Kosa lake la tisa;**

Amesema  katika ukurasa huo wa pili;

[..na pia ameandika akimnukuu Qattan kuwa Habib alikuwa si mtu wa kufuatwa hata kidogo.]!

**Jawabu yetu;**

Sawasawa ni al Qattan.Lakini pia huwenda likawa hili ni kosa la kiufundi kwahiyo halidhuru, lakini tunakumbusha tu,.
Na kosa lenyewe liko katika hayo maneno aliyo nasibishiwa al Qattan.

Kwa ufupi ni kwamba sheikh huyo wa Buguruni hakuyaelewa maneno ya sheikh mwenzie,na maneno yenyewe yako hivi;

...ولا يتابع عليه,له غير حديث عن عطاء

Maana yake ni kwamba;

Habib ana hadihti kutoka kwa Atwaa isiyo kuwa moja(nyingi) ambazo hakufuatiwa (hakushirikiana) na yoyote-amezipokea peke yake-
Kwa lugha ya kitaalamu wanasema;

Habib hana mutaabaa kutoka kwa Atwaa.

Kwahiyo siyo kweli alivyosema sheikh wa Buguruni kwamba Habib hafai kufuatwa !
Hivi kweli mtu kama huyu asiyejuwa makusudio ya maneno ya maulamaa anastahiki naye kuwa ni msemaji wa waislamu,tena kwa kadhia nzito kama hii ?
Msiba ulioje ! اللهم غفرا

Halafu kwa ufahamu wake huu uliopinda anawatia kasoro maulamaa wakubwa kama hawa!
Lakini kitambo alishasema mshairi kwamba;

وكم من عائب قولا صحيحا * وآفته من فهم سقيم

Na miongoni mwa maulamaa walio jeruhiwa na muhadithi huyu wa Buguruni kwa mnyamani ni amirul muumina fil hadithi al Imamu Sufiyan bin Said bin mas'rouq Athaury.

Kwa sababu ya ufahamu mbaya wa muhadithi huyo,katika kuyafahamu maneno ya maulamaa.

Hebu tumuangalie Al hafidh Ibi Hajar al As'qalany anatuambia nini kuhusu Sufiyan?

Amesema Ibin Hajar;

**[ Haafidhun,faqiihun,Aabidun,Imaamun,Hujjatun.].**

[Sufiyan ni mwanawachuoni mwenye kuhifadhi,mtambuzi wa fiq'hi,mwenye kufanya ibada,ni Imamu,tena ni Hoja.].

Sheikh wetu wa Buguruni yeye akasema hapana,ndipo akayachukua maneno ya Ibin Mubarak yasemayo [kaana yudallisu] kwa maana ya kudanganya !

Fuatilia mfululizo wa makala zetu;

HII NDIYO DAAWA YETU JUU YA UFAHAMU WA SALAF SWALIH

- **1,2,3.) Athari mbaya ya Uzushi katika uislamu.**

- **4,)Uharamu wa kuyajengea makaburi**
  (ni hii iliyo mikononi mwako).

- **5)Uharamu wa kuyajengea makaburi.**
  **Majibu na maelezo**

- **6)Uharamu wa kuswali kuelekea makaburi.**

Tanbihi;

1-Tafadhali usikose makala ifuatayo ni muhimu.

2-Ukiipata makala hii toa copy nyingine na umpe mwenzako kwa lengo la kueneza ujumbe

**وصلى الله وسلم وبارك على محمد وعلى آله وصحبه أجمعين.**
**وآخر دعوانا أن الحمد لله رب العالمين.**